# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

Mwaka XXI – N. 7, Julai/Agosti 2019


Mhariri

## Wito kwa Kanisa la Wanawake

Siku moja tu imepita tangu Mkesha wa Pentekoste na maneno ya Papa Francis, aliyotangaza wakati wa mahubiri kwenye Uwanja wa Mt. Petro yanaendelea kusikika katika akili lakini zaidi sana kwenye moyo. Ni kama yanataka kutengeneza nafasi, kujitokeza, ili kuchukua umbo na mwili. Alikusanya pamoja Kanisa lote la Roma ili kusali pamoja hadharani. Kama Mama wa Makanisa yote, kielelezo na ishara ya umoja wake, anaitwa kujifanya tumbo linalokaribisha, kusikiliza kilio cha Roho ambacho kinatoka kwa maskini. Anaalikwa kushinda hofu na, kama akina mama wote, kujiweka kwenye mstari wa mbele ili kutetea, kulinda na kurejesha matumaini.

Ni Kanisa lenye sifa hasa za kimama, za mwanamke. Ni wakati wa Roho ambaye anatuita kuweka katika vitendo vipaji vyetu, hali yetu ya kike, namna yetu ya hisia na kuelewa hali halisi kwa ajili ya kutoa jibu ambalo linahusisha moyo.

Halijali maslahi au faida ya kibinafsi, uzalishaji, utendaji, ufanisi, tunu zote ambazo zinakuza ubinadamu wetu; Kanisa linatangaza uwepo wetu, huruma yetu, nafsi yetu.

Kanisa la wanawake ni la Maria ambaye amelizaa chini ya msalaba, akijiunga na sadaka kamili ya Mwanae, mwanzo wa ubinadamu mpya, lile la damu ambalo huchangamotisha umati wa watu dhaifu wenye uhakika wa kuponywa, la mwanamke Msamaria kisimani, ambaye anafungua majadiliano na mgeni, anajihusisha katika majadiliano hadi kufikia ukweli wa yeye mwenyewe, la Maria wa Bethania ambaye huinama kuosha miguu ya mwalimu, kwa tendo la ibada na shukrani na lile la Maria Magdalena ambaye kutoka kaburi tupu anakimbia kwa sababu hawezi kujizuia kutangaza siri ambayo ameishuhudia.

Kama Waabuduo tunapokea mwaliko huu kila siku kwa kufanya chaguzi ambazo zinatufanya sisi kutoa kipaumbele kwa tunu zetu. Mpango wa semina kwa ajili ya wahasibu wenye mada uso wa kibinadamu wa uchumi, mang'amuzi ya mapokezi ya maskini katika jamuiya zetu na yale ya huduma, ya umakini kwa wazee na ya kuchukua hatua katika ulinzi wa viumbe ni hatua halisi zinazooneka ambazo zinatuita ili kujiimarisha na kusaidiana katika safari ya mabadiliko ... kwa ajili ya Kanisa la wanawake ambalo linazaa maisha mapya.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Mhutasari


*Mhariri*
- Wito kwa Kanisa la Wanawake 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Jumuiya ASC "inayotoka" 2

*Toka Ulimwengu ASC*
- "Mimi hapa, Bwana…" 3
- Komunyo ya Kwanza 4
- Kumbukumbu ya Miaka 16 tangu kutangazwa kuwa Mt. MDM 4
- Bustani ndani ya mapipa 5
- Kuwekwa taji katika Nyumba ya Watoto Wakatoliki (CCH) Mei 6
- Tuzo ya Heshima kwa Sista Charlotte 7
- Mang'amuzi ya kufanya angalau mara moja katika maisha! 8
- Uso wa kibinadamu wa uchumi 9
- Mang'amuzi mazuri ya furaha 10
- Miaka 125 ya uwepo wa ASC Bihać 11

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Pamoja kwa ajili ya Maisha, Heshima na Haki za kibinadamu 12

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 13
- Sherehe za kuzaliwa : tunasherehekea maisha 13
- Sherehe za Nadhiri za Kitawa 13
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 14

## Jumuiya ASC "inayotoka"



Tangu Januari 2019, Jumuiya ya Kimataifa ya Nyumba Kuu imekaribisha familia yenye asili ya Siria: mama na wasichana wawili, waliokuja nchini Italia shukrani kwa mradi wa vituo vya kibinadamu vinavyohamasishwa na Jumuiya ya Mtakatifu Egidio. Hili ndilo jibu ambalo Uongozi Mkuu, pamoja na Jumuiya ya Kimataifa, walitaka kutoa kwa wahamiaji kwa kushirikiana na taasisi nyingine zilizopo katika Kanisa. Kwa kweli, mradi wa vituo vya kibinadamu vinafanya kazi ili kupata kibali cha kimataifa kinachohitajika kuhamisha watu au familia zilizo katika mazingira hatari kiafya na kimaisha kutoka makambi ya wakimbizi ya Libya na kuwakaribisha katika nchi yetu. Siham, Mariana na Marina, katika mateso yao, katika hali ya kutokuwa na nguvu na katika hali ya upweke wamekuwa miongoni mwa wale wenye bahati. Baada ya kufika Roma, leo wanaendelea kuwa pamoja na Jumuiya ileile ya Mtakatifu Egidio katika mradi ambao unalenga kusaidia mshikamano wa wahamiaji, kupitia ufundishaji wa lugha, maandalizi ya nyaraka za kisheria, utoaji wa kozi za kitaaluma, ili waweze kuingizwa katika hali mpya ya mapokezi. Jumuiya ya Mtakatifu Egidio kupitia mawakala wake huratibu kazi na mipango, kutoa misaada na kuwaongoza hata wale waliokabidhiwa kwa Waabuduo.

Wasichana hawa, leo wanajishughulisha na kujifunza lugha, wanatumia njia zote zilizopo za kufanya mazoezi ya Kiitaliano, wakijenga mahusiano ya nje, wenye utayari wa kusaidia kwenye jamumuiya kulingana na uwezo wao na kazi zao, wanatoa huduma ya kujitolea katika kituo hicho cha Mtakatifu Egidio au parokiani pamoja na wahamiaji wengine.

Wasichana hawa watatu watakaa pamoja nasi kwa mwaka mmoja na siyo wao tu pekee wanaofaidika kutokana na mapokezi yetu na ukarimu wetu bali hata sisi jumuiya ya kimataifa tunafaidika kutoka kwao.

Kwa kweli, jibu kwa maombi ya Kanisa yaliyotolewa na Papa Francis na lile la Hati ya Mkutano Mkuu wa 2017, kuwa jibu la huruma na upatanisho ambalo tunaishi katika ushirika na maskini, waliotengwa na wale wanaoishi pembezoni ... Kuwa moyo ulio makini kwa kilio cha damu, kutunza nyumba yetu ya pamoja na kulinda maisha na heshima ya kila mtu, kunatufanya tujue kuwa hili ni fumbo la Pasaka, kwa sababu kwa upande mmoja linatupa nafasi ya kutoka ndani mwetu wenyewe, kutoka katika nafasi zetu na salama wetu, kwa upande mwingine kujenga hali muhimu ndani yetu za kugundua rasilimali za ndani zaidi: ni haya mabadiliko ambayo huzaa maisha.

Zaidi ya hayo, jumuiya ya Nyumba Kuu, Jumuiya ya Kimataifa, imetajirishwa na uwepo mpya. Historia ya Siham na binti zake wawili, kila siku inatufanya tusikie kilio cha haki kinachojitokeza kutoka kwa watu walio vitani, kutoka kwenye ile sehemu ya binadamu ambaye ni mwathirika wa ubaguzi na hofu ya ulimwengu wote. Wanatusaidia na kutusukuma kwenye sala ya maombezi halisi na yanayoonekana, wanatuita upya kwenye hitaji la uongofu wa kweli wa moyo kwa sababu hutufanya kuwa majirani. Uwepo wao unatukumbusha kwamba sisi ni familia moja, familia ya kibinadamu, na kwamba wajibu wa kujenga familia hii ni nguvu inayotuongoza sisi kuamini kuwa kutakuwa na wakati ujao na kwamba huo utakuwa bora.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

Eneo la Bara: Africa
Region ya Tanzania

## *"Mimi hapa Bwana ..."*



Tunamshukuru Mungu kwa upendo wake katika siku hii ya pekee ambapo tumefunga nadhiri za kwanza. Hii ni siku ya pekee kwetu na kwa Region yetu kupata wanashirika wapya.

Baba Askofu Beatus Kinyaiya wa Jimbo Kuu la Dodoma aliongoza Misa, pamoja na mapadre wengi. Tuliguswa na mahubiri yake alipotuasa kuwa "Tuchuchumilie utakatifu kwa kuwa Baba yetu wa mbinguni ni Mtakatifu. Alisema kuwa Sikukuu kuu katika kanisa ni Pasaka kwa sababu tunasherehekea ukombozi wetu kupitia mateso na ufufuko wa Kristo ambao Mtakatifu Maria De Mattias aliushi na kuufundisha kwa moyo wake wote. Kilichomgusa sana Mt. Maria De Mattias kilikuwa ni upendo mkuu wa Yesu aliyeteseka kwa ajili ya kutukomboa sisi. Ndiyo maana roho ya shirika ni Upendo kwa Mungu na kwa jirani.

Swali la Yesu kwa Petro mara tatu, je wanipenda? Yesu alifanya hivyo ili kumpa Petro fursa ya kutafakari zaidi kile alichokuwa akitamka. Alituambia leo "mnajonga Altareni kufunga nadhiri kufuatana na karama ya Mt. Maria De Mattias, hivyo mnaitwa kumfuata Yesu kwa fuata nyayo za Mtakatifu Maria De Mattias."



Akirejea somo la Injili; alisema "Maria Magdalena baada ya kifo cha Kristo alikuwa na mahangaiko kwa sababu alikuwa na upendo mkubwa na wa kweli kwa Kristo. Kwa hiyo alipomwona Yesu Mfufuka alitaka kumng'ng'ania: lakini Yesu hakumruhusu, badala yake alimtuma kwa wanafunzi kupeleka Habari Njema. Masista wateule mjifunze kwa Maria Magdalena, kila mtakayekutana naye mhudumieni kwa upendo." Askofu Mkuu alisisitiza kuwa tunapaswa kumng'angania Yesu lakini bila kusahau kuwa tuna wajibu wa kwenda kukutana na ndugu zetu wahitaji, ili kuwapelekea Habari Njema. Kama alivyofanya Mtakatifu Maria De Mattias, tunapaswa kuwahudumia watu wote kwa upendo. Alituhimiza zaidi kuwa tusiogope kusimamia ukweli, kuwa watu wa sala, kazi na kuwapenda watu wote, na tuwe vyombo vya kazi ya ukombozi iliyofanywa na Yesu.



Tunapenda kumshukuru Mungu kwa zawadi ya wito. Tunawashukuru wazazi na walezi na ninyi yote dada zetu wapendwa ASC popote mlipo kwa upendo wenu na sala zenu kwa ajili yetu. Mungu aendelee kuwajalia baraka zake.

***Sr. Coleta John, Sr. Joanitha Emmanuel,***
***Sr. Maria Anatoli na Sr. Rosina Respicius, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Foundation ya Argentina

## Komunyo ya Kwanza

### Chuo cha Damu Azizi

Mnamo Mei 11, wanafunzi wa mwaka wa 5 wa mkondo, A, B, C, wa Chuo cha Damu ya Azizi walimpokea Yesu kwa mara ya kwanza, baada ya kozi na maandalizi ya miaka 2 yaliyofanywa na makatekista, wazazi, walimu na masista.

Wazazi walishiriki katika shughuli za kila mwezi na kufanya mikutano pamoja ili kusindikiza safari ya imani ya watoto wao . Wanafunzi walikuwa wahusika kwa maandalizi ya liturjia, maandalizi ya altare, kupeleka Neno, mishumaa, maua, vipeperushi, na wakati wa matoleo vichupa na mkate.





Walishiriki kusoma Neno la Mungu na kujitolea kwa Mama yetu Maria Mtakatifu.

Wakati wa kumpokea Yesu, ambapo ni hatua muhimu zaidi, kwa mara ya kwanza walionekana kuwa na furaha sana.

Walioshiriki Misa ni wafanyakazi, viongozi, walimu, Makatekista na idadi kubwa ya ndugu, kwa sababu ndani ya miezi mitatu jumla ya idadi ya watoto ilikuwa 100.

Damu ya Kristo ijaze mioyo ya watoto hawa ili waweze kuwa daraja la upendo na rehema kwa watoto wengine wa Shule.

***Sr Susana Misermont, ASC***

Region ya Manaus

## Kumbukumbu ya Miaka 16 tangu kutangazwa kuwa Mt. MDM

*Jumuiya ASC ya Belem inasimulia…*

Mnamo mwezi Mei 18, jumuiya yangu ya Bibi yetu wa Guadalupe, huko Belem, katika Jimbo la Pará, tulifanya kumbukumbu ya mwaka wa 16 tangu kutangazwa Mt. Maria De Mattias. Padre Arcelino, mkuu wa Mapadri wa Vicarieti ya Brazil ya Wamisionari CPPS, aliongoza adhimisho la Misa, pamoja na Padri Lucas Fuertes, CPPS, ambaye, anahitaji matibabu, ni mgonjwa wetu katika hospitali ya Guadalupe. Padri Arcelino ni mmishonari huko Altamira na alishukuru kwa mwaliko wetu wa kusherehekea sikukuu ya Maria De Mattias pamoja nasi.

Kwa ajili ya tukio hili, Sr. Jocilene aliandaa kitabu kipya cha nyimbo. Pamoja uwepo wa mapadri hawa walikuwepo pia Zilda, mwanamke mlei rafiki wa masista na wamisionari, padri Viganò, CPPS, anayeishi Altamira anayemtunza Padre Lucas na Bi Valeria, mwenye ibada kwa Damu Azizi, pamoja na binti yake wa miaka 12, Maria Eduarda; ambaye alikuwa na kitita kikubwa cha maua ambayo aliyagawa kwa kila mmoja na wakati wa matoleo alitualika kuyatolea altareni kwa Yesu ili kutoa shukrani kwa zawadi ya maisha yetu kama Waabuduo.

Baada ya mahubiri ya Misa, Padre Arcelino aliniomba kusimulia sikukuu ya kutangazwa kuwa Mtakatifu Mt. M. De Mattias. Hata kama siku hiyo ya tarehe 18, 2003 sikuwapo katika Kiwanja cha Mt. Petro, huko Roma, kwa sababu wakati huo huo na siku hiyo hiyo yalichimbuliwa masalia ya Sr. Serafina Cinque huko Manaus, nilikuwa nimesikia mengi kuhusu kutangazwa kuwa Mtakatifu, kutoka kwa masista ambao walishiriki na kutoka kwenye makala zilizochapishwa katika magazeti na majarida ya ASC.

Nilijisikia fahari na nilifurahi kuweza kupata nafasi ya kusimulia kwa shauku juu ya yale yaliyosimuliwa na watu waliokuwa katika Uwanja ya Mt. Petro, juu ya masimulizi ya muujiza wa kijana Vladimir, ambaye kwa uponyaji wake kuliwezesha adhimisho la kutangazwa mtakatifu na maelezo mengine mengi ya pekee. Katibu wa Regiona, Sr. Beth, aliandaa sala ya siku tatu kwa ajili ya maandalizi ya sherehe na adhimisho la misa. Nilimsaidia Sr. Maria José, msakristia, kuandaa misa. Nilisali na kumshukuru Sr. Maria Paniccia ambaye alifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kutangazwa Mtakatifu Mwanzilishi wetu. Sr. Marlene alipiga picha kadhaa, na kila mmoja wetu alijisikia kuwa mshiriki katika tukio hili la kumbukumbu. Kwa ajili ya kukumbuka ya miaka ya 185 ya kuanzishwa Shirika, niliandika makala katika gazeti la Jimbo la Belem ambalo lilichapishwa hapa miezi michache iliyopita.

Tuliimba nyimbo kwa Mwanzilishi wetu mpendwa ambazo sisi wenyewe tulizitunga na tukamaliza tukio hilo kwa chakula cha mchana cha kufurahisha na tunamshukuru Mungu kwa yote.



**Sr. Marilia Menezes, ASC**
*Region ya USA*

## Bustani ndani ya mapipa

Pipa ni pipa tu mpaka hapo ambapo si bustani.

Hii ni hadithi ya mapipa sita ya bluu ambayo sasa hutoa nafasi ya bustani kwa masista sita katika Nyumba ya Ruma. Kilimo cha bustani kimekuwa ishara inayowapambanua masista wa Ruma kwa miaka mingi. Wakati ardhi ya bustani inapotikisika, Ardhi inataja majina ya Mary Edwin, Teodolinda, Sebastian, Edwiga, Vera, Dorothy Ann, Mary Edith, Janis na wengine.

Mapipa haya sasa yanazunguka nguzo ambako alikuwepo Mt. Clementi na kutoa nafasi ambapo masista wanaweza kulima bustani wakiwa wamesimama. Mboga za majani zinapendeza kweli: masista Lucille Kern na Frances Newton wanalima figiri, sista Celine Birk analima spinachi, sista Anne Irose analima kabichi na sista Alan Wurth analima vitunguu na saladi.

Mnamo mwezi Mei, jumuiya ASC ilifurahia figiri, vitunguu vibichi na spinachi.

**Sr. M. Alan Wurth, ASC**



# kuwekwa jaji katika Nyumba ya watoto Wakatoliki (CCH) Mei

Waabuduo wengi wa eneo la Ruma walipita kwenye Nyumba ya Watoto Katoliki huko Alton, Illinois, wakati wa miaka yao ya utumishi wa kazi kabla ya 1984. tangu Waabuduo walipondoka huko, Walei Wakatoliki wa Jimbo la Springfield waliendelea kuwahudumikia watoto wenye mahitaji.

Ingawa wafanyakazi wote siyo Wakatoliki, hali na shughuli zinaendana na maneno ya Kristo: “Waache watoto waje kwangu”. Kama ilivyokuwa siku zile Waabuduo walipokuwa kwenye CCH, watoto wenye mahitaji zaidi wanaendelea kuhudumiwa. Mipango inayotolewa na kituo ni mitatu:

- Shule ya kutwa kwa watoto wenye elimu maalum, madarasa 1-12;
- Mpango wa makazi kwa wavulana na wasichana ambao wanahitaji kubadili maamuzi waliyofanya;
- Mpango wa kuandaa vijana kuishi kwa kujitegemea.



Kupitia mmoja wa walimu wa CCH, Mei 3, Sr. Olivia Woltering na Sr. Rachel Lawler walipokea mwaliko wa kushiriki katika maonyesho ya sanamu ya Mama yetu wa Fatima. Masista hawa wawili walifanya kazi katika kituo kwa miaka mingi. Sista Rachel alifanya kazi katika kituo kwa miaka 21 kabla ya kwenda Liberia, Afrika.

Mwaka jana, Sanamu ya Bikira Maria ilikuwa imeharibiwa kwa namna ambayo isingeweza kurekebishwa tena.

Jimbo ambalo ndilo mmiliki wa majengo, liliibadilisha na nyingine kutoka Italia. Askofu alikuja kubariki sanamu mpya mwezi uliopita, Aprili 1. Sr. Rachel, Sr. Frances Newton, Sr. Hedwig Neff na Sr. Olivia, walisaidia tukio hili kwa kutoa huduma huko.

Mnamo Mei 3, kwa ajili ya kuisimika, Padri Stone wa Kanisa la Mt. Petro na Paulo alifanya adhimisho la ibada na mvulana wa shule aliweka taji ya maua juu ya kichwa cha sanamu ya Maria, kutokana na kwamba hakuna wasichana katika darasa la juu.

Mwanzo, kwa mujibu wa masimulizi ambayo marehemu Sr. Remigia aliyasimulia kwa Sista Rachel, sanamu ya Mama Yetu wa Fatima ilikuwa ndani ya jengo na iliharibiwa katika tukio la kawaida la kimbunga hapo Alton.

Wakati Sista M. Elizabeth Utar alipokuwa mkuu na msimamizi wa kituo, sanamu ya Mama Yetu wa Fatima iliwekwa kwenye mlango wa shule (iliharibiwa mwaka jana).

Sista Lucille Kern anakumbuka kwamba wakati sanamu ilipowekwa nje, wakati hali ya hewa ilikuwa nzuri, kwa kawaida jioni masista na watoto walikuwa wanakusanyika kuizunguka ili kusali rozari. Historia ya kimbunga na kusanyiko karibu na sanamu kwa ajili ya kusali imeelezwa katika daftari la historia ya CCH.

Kimbunga huko Alton ni adimu kutokea, lakini mafuriko ni ya kawaida kwa sababu mji umepitiwa na mto Mississippi. Mwezi Aprili tarehe 1 na mwezi Mei tarehe 3, Mississippi ilifikia kiwango cha Road Great Road, barabara inayoanzia Alton hadi Grafton, Illinois.

Mazingira yaliyoko karibu na Broadway na barabara za serikali za Alton huwa na alama za urefu tofauti wa mafuriko yaliyotokea katika miaka ya nyuma. Mto huo ulijaa kiasi cha kutosha kuweza kuacha alama yake mwaka huu.

***Sr. Olivia Woltering, ASC***

# Tuzo ya heshima kwa Sista Charlotte

Sr. Charlotte Rohrbach, ASC alipata tuzo ya heshima ya udaktari mwezi uliopita kutoka Chuo Kikuu cha Newman.

Kila mwaka tuzo ya digrii ya heshima hutolewa kwa mwanachama mahiri na mwenye ufanisi wa jumuiya pana ya Newman, ambaye maisha yake na kazi zinaonyesha majitoleo ya mfano kati ya moja ya tunu msingi za chuo kikuu: utambulisho wa kikatoliki, utamaduni wa huduma, ubora wa kitaaluma na mtazamo wa kimataifa.

Sista Charlotte alipokea heshima kwa kujitolea kwake kwa Chuo Kikuu cha Newman na mafundisho ya elimu ya juu ya Kikatoliki , pamoja na mifano yake yenye nguvu ya imani ya Kikatoliki.

kipindi chake huko Newman, Sista Charlotte mefanya kazi mbalimbali kama profesa wa historia, mkuu wa kitivo, mkurugenzi wa chama cha wanafunzi, mkurugenzi wa idara ya kichungaji, mkurugenzi wa wakufunzi, mkurugensi wa utafiti wa nje ingawa kwa muda mfupi na mkurugenzi mtendaji.

Hapa ni maneno yake wakati wa kupokea tuzo ya digrii ya heshima.

I. Maneno ya utangulizi

Nilifanya! Nia: wakati nilipokuwa naenda NU, 2/05, nilianguka na kuvunja mfupa wa paja. Nimepata tena elimu ya anatomia ya miaka yangu ya chuo kikuu. Sasa naweza kuongeza nyingine "mang'amuzi ya kuvutia na ya kuchochea" kwenye historia ya maisha yangu.

Asubuhi hii nina moyo uliojaa furaha na shukrani kwa sababu ya chuo changu kikuu ambacho kinanipa heshimu hii ya digrii ya udaktari. Nilikuwa na muda mwingi wa kutafakari juu ya kile ninachotaka kusema leo; ni hatari kutoa hata kama ni dakika chache za kushirikisha kwa mwongeaji .... Kwangu na, nadhani pia kwako, maisha ni swali la mahusiano. Mahusiano yangu yamejikita katika jamuiya tatu ambazo mimi nimekuwa chini yake: familia yangu ya damu, familia yangu ya kitawa na familia yangu ya Chuo Kikuu cha Newman. Nadhani sisi wote tuna wawakilishi kutoka familia hizi – mimi ninao.

II. Familia yangu ya damu

Kikundi changu cha kwanza cha kifungo. Ningeweza kuandika kitabu, lakini badala yake nataka kuwaambia hadithi kuhusu somo ambalo kamwe sitalisahau.

Nilikuwa nimehitimu digrii yangu ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Mt. Louis cha Mafunzo ya Marekani, muda mfupi kabla ya Krismasi. Kaka yangu mdogo alinizawadia sweta nyeusi yenye herufi za dhahabu ambazo zilisomeka Super NO ONE (hakuna aliye bora). Kwa kweli nilijifunza somo muhimu la unyenyekevu – ninaendelea kujifunza somo hili kila siku.

III. Familia yangu ya kitawa

Wakati wa kukamilisha shahada yangu, nilijiunga na Waabuduo Damu ya Kristo, ambao walianzisha na kufadhili Chuo Kikuu cha Newman.

Kipindi chote cha miaka yangu mingi ya mahusiano na kikundi hiki kikubwa cha wanawake, nilipewa elimu, nilifundishwa tunu ya maisha ya jamuiya, nilijifunza utume wangu binafsi ambao ninaitwa kila siku kuuishi. Bado naufanya tena kwa kusimulia.

Mafundisho daima yamekuwa shauku yangu – kwa kusimulia maisha kama hivi nilivyoyaishi, nimeyaishi na ninaweza kuyaishi. Elimu rasmi ilikuwa mhimu kwangu ili kutimiza ndoto yangu ya kuwa mwalimu. Niliombwa kuendelea na elimu yangu rasmi ambayo ilijumuisha pia utafiti ambao mara kwa mara niliuona kama kupoteza muda. Wanajumuiya wa jumuiya yangu walinitia moyo ili kutimiza ndoto na kufanya hamu yangu iwe kwa ajili ya utume na huduma yangu ya maisha.

IV. Familia yangu Chuo Kikuu cha Newman

Karibu miaka 50 ya maisha yangu yametumika Newman kama mwanafunzi, mwanachuo na mfanyakazi. Kuna watu wengi ambao wangeweza kunilipa ingawa hawasimulii hadithi zaidi. Nimebashiri kitu – nimeamua kuchukua fedha na kupanga likizo kubwa!

Mahusiano yangu ya miaka hii ni muhimu kweli - niwezaje kuchagua watu ambao wanaweza kuhusiana nami? Hazina zinadumu maisha yote – ndivyo zilivyo zangu!

V. Maneno ya kumalizia

Una jumuiya yako, mahusiano yako. Daima yahifadhi kama tunu.

Leo wanakusherehekea. Waache wakusherehekee, umefikia heshima kubwa. Lakini daima kumbuka kusimama kwenye vitu muhimu zaidi.

kwa mara nyingine tena, shukrani kwa Chuo Kikuu cha Newman kwa heshima ya leo. Narudi kwenye ofisi yangu bila kurefusha mambo zaidi.

***Cheryl Wittenauer***



# Mang'amuzi ya kufanya angalau mara moja katika maisha!

Mimi mara kwa mara ninapokea mwaliko wa kuhudumia kwenye Utume wa Matibabu ya Shirika kwa sababu ninaamini kuwa ni muhimu kushirikisha kipaji ambacho Mungu amenijalia. Utume huu wa matibabu kwa kawaida wanaufanyika kwenye nyumban yao ya kitume au katika maeneo ya karibu. Mara hii, hata hivyo, kutoka tarehe 19 hadi 25 Mei 2019 utume wa matibabu ulifanyika kisiwani katikati ya Philippine na ilikuwa ni wakati wa pekee kweli.

Tulilazimika kusafiri kupitia ardhini na baharini ili kufika Mkoa wa Romblon, katika visiwa vya Tablas na Alad, mahali pa utume wetu wa matibabu na kuanza kazi yetu ya matibabu.

HukoTablas, kisiwa kilichochaguliwa, kuna jamuiya nzuri: CARMEN, ambapo watu ni wema, wakarimu na wenye upendo, wanaongozwa na kulindwa na Msimamizi Mtakatifu wao - "Mama yetu wa Mlima Karmeli." Parokia inasimamiwa na Padri, mcha Mungu, mwajibikaji na mwenye nguvu, Padri Diong. Wanaparokia wote ni wema sana na walitukaribisha kwa zamu katika huduma, katika milo yetu yote, kati ya Carmen nyingine kuna mji alikozaliwa Sr. Flor Manga. ASC - tuligudua mazingira yanayozunguka Carmen na tulifurahi kuona madhari ya mji kutoka juu ya mlima wenye urefu wa futi 580 ambapo picha ya Mama Yetu wa Guadalupe inalindwa kwenye kanisa ndogo lakini ikiwa imehifadhiwa vizuri.Tulijaribu pia kwenda chini ya maji pamoja na watu mbalimbali, mang'amuzi haya yalitufanya tufahamu kuwa kweli ni mchezo wa kuvutia lakini pia unaoumiza na hatari.

Utume wa matibabu huko Carmen umefanikiwa sana, tunaamini tumewahudumia watu wa Mungu kwa kujitolea kwa upendo. Wagonjwa ambao walikuja kwa ajili ya kupata ushauri, walipokea dawa za bure; wamefika pia magonjwa mbalimbali kama vile: wenye shinikizo la damu, matatizo ya tumbo kwa watu wazima, wenye mafua na magonjwa ya ngozi na utapiamlo kwa watoto. DoktaWeng pia alifaidi fursa ya kutoa elimu ya usafi na kwa namna ya pekee kuhusu shinikizo la damu.

Wote ambao wamefaidika na huduma yetu wameondoka wakiwa wameridhika wakitoa shukrani zao kwa timu ya SMDMMC na kuwaomba tena na tena kurudi kwa mara nyingine ...

Pia katika Kisiwa cha Alad Romblon, tulihudumia jamii katika parokia ya Mtakatifu Vincent Ferrer. Paroko Fr. Alan Christopher Montajo, kijana, mwajibikaji na mwenye nguvu, alituongoza kwa kutuonyesha maeneo mazuri zaidi mahali hapa. Wakati tukiwa pale kwa siku 2, Padri Alan alituwezesha kutembelea visiwa vya karibu vya Cobrador na Sandbar. Wakazi wa maeneo hayo ni wanyenyekevu, wema na washika dini. Misa huadhimishwa saa kumi na moja asubuhi na wengi wanakuja kanisani kusali.

Asubuhi ya Mei 24, 2019, tulipofika Alad, tulikuwa na wavulana waliotahiriwa 20 wenye umri wa miaka 10 hadi 13, hapa Philippine tunatahiri watoto wanaoishi wakati huu kwa fahari, kama ishara ya kutoka ktika umri wa kubalehe.

Kuondoka katika eneo lenye baraka, kutoka mji wa Quezon na kushirikiana na wale walio katika uhitaji kweli ni njia ya kumpenda na kumtumikia Mungu. UTUKUFU UWE KWA MUNGU!

***LOURDES S.M. SARMIENTO M.D. ROMBLON***



# Uso wa kibinadamu wa Uchumi



"Wamisionari ni wanaume na wanawake mashujaa ambao husikia wito wa Bwana na kuondoka nyumbani kwa ajili ya jambo fulani. Kwa ujasiri huenda mbali zaidi ya maeneo yao ya faraja hata kama ni nyumbani tayari hufurahia uhakika wa kichumi, kijamii na kitawa. Hawana uhakika juu ya njia ya kufuata, lakini wana ujasiri wa kuiacha pwani, kwa kawaida, wanategemea neema yake ". (Kutoka gazeti MAGOET).

Bwana akamwambia Ibrahimu: toka wewe katika nchi yako na jamaa zako na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha (Mwanzo.12.1); Ibrahimu akiwa na imani thabiti anaenda katika nchi asiyoijua bila kuwa na mtu wa uhakika wa kumwongoza, hivyo hivyo kama Musa. Wakati Yesu anawaita wanafunzi wa kwanza, anawataka kuacha familia zao na kile walichokuwa nacho, ikiwa ni pamoja na nyavu, na kumfuata wakiwa masikini kama Yesu Mwalimu wao. Katika ulimwengu wenye athari za nguvu, kazi, sifa, mafanikio, mapato, mali, mamlaka na umaarufu, si rahisi kusema Amina kwa mwaliko wa kimapinduzi wa Bwana, mbele ya hali halisi ya kila Region.

Mkutano uliofanyika huko Roma, kwenye Nyumba Kuu, kuanzia tarehe 13 hadi 18 Mei, ulikuwa ni fursa nzuri kwa wahasibu kutoka sehemu mbalimbali za Shirika kuungana na kushirikishana hali halisi za Region zao, rasilimali watu, matumaini, changamoto na matarajio. Semina kwa wahasibu wa Region na Foundation ASC, yenye mada: "uso wa kibinadamu wa Uchumi", ilikuwa msaada mkubwa kwa kuelewa na kuimarisha usimamizi wa kiinjili wa mali. Tumehamasishwa kuwa na uelewa wa uso wa kibinadamu wa usimamizi ambao hujionyesha katika uwezo wa kuratibu michakato, kutunza watu na kukabiliana na wale ambao huleta vikwazo katika usimamizi mzuri wa mali. Sisi siyo watendaji tu wanaohusika na kazi na usimamizi wa mali. Kama mtumishi mwaminifu wa Injili pia tumeitwa kufanya kazi ya usimamizi kwa namna ya uajibikaji na umahiri.

Kila Mwabuduo anaitwa kuwa "mhasibu", msimamizi wa aina mbalimbali za neema za Mungu zinazojionyesha katika vipaji vya kibinafsi vya kila mtu, ili kuleta maboresho kwa faida ya wote. Ninashukuru kwa fursa ya semina hii ambayo kwangu ilikuwa ni yenye mang'amuzi yenye utajiri mkubwa, zaidi ya yote kwa sababu ilikuwa msingi wa utafiti na kuelewa kwa undani hati ya kanisa "Uchumi katika huduma ya Karama na Utume".



**_Sr. Lalitha Varakukalayil, ASC_**

# Mang'amuzi mazuri ya furaha





Jubilei ni sherehe ya uaminifu wa Mungu katika maisha yetu na ya safari halisi ya maisha yetu, ni wakati wa kutoa shukrani zetu kwa Mungu na kwa wengine, ni wakati wa kusherehekea uaminifu wetu kwa Mungu, kumbukumbu ya magumu na ya mapambano ambayo tumeyaishi katika maisha yetu na halafu ni sikukuu ya yote ambayo tumeyafurahia katika safari yetu ya maisha.

"Moyo wangu unatangaza ukuu wa Bwana na roho yangu hufurahi katika Mungu Mwokozi wangu" (Lk 1: 4-47). Ndiyo, nikijiunga na Maria Mtakatifu sana, pamoja na Sr. Mini Vadakumchery Ninamshukuru Bwana kwa upendo wake na baraka zake. Mioyo yetu imejaa furaha kwa zawadi ya wito tuliopewa. Wito huu wa pekee katika maisha ya kitawa umetufanya tuwe karibu sana na Yesu. Ni ukweli wazi na mang'amuzi yetu kwamba Mungu ni mwaminifu daima kwa ahadi zake katika maisha yetu. Kwa kweli amekuwa ni Mungu mwenye kujali, mwenye upendo, mwenye fadhili na mwenye ukarimu kwetu.

Ilikuwa ni wakati mzuri sana ambao Mungu aliutayarisha ili tuweze kuona miaka yetu 25 ya maisha ya kitawa katika kanisa na ndani ya familia ASC. Katika kipindi hiki cha miaka 25 tuliweza kutambua baraka za Bwana, za mchango ambao jamii, familia yetu na familia ASC waliotoa katika maisha yetu na ukuaji wetu na mchango ambao tumeutoa kwa wengine. Kipindi cha miaka hii 25, tumehisi kubekwa na Mungu katika mikono yake, na kutunzwa kama mboni za macho yake. Alitusaidia katika shida zetu zote, wakati wa furaha, nyakati za mashaka, maumivu na katika upweke.

Tunawashukuru watu wote ambao Mungu amewatumia kama zana za kutuunda na kututengeneza ili kuwa hivi tulivyo. Tunawashukuru sana wote, hasa wazazi wetu, ndugu, majirani, wakuu, watu ambao wametuongoza katika kutambua wito wetu, walezi, wanafamilia ASC, walimu na marafiki. Leo, tunafurahia uchaguzi wetu wa maisha ya wakfu, tunajitahidi kuridhika kwa kile tulichopokea na kwa jinsi tulivyo. Shirika letu, familia ASC, ambayo tunajisikia kuwa chini yake, ilitukaribisha katika hali yetu ya kutokuwa na kitu chochote na kututunza. Sherehe hii imetufanya tufurahi sana na tunataka kutoa shukrani zetu kwa Mungu na kwa wote wanaotuzunguka. Tunajiweka wenyewe kwenye huruma ya Mungu na tunatumainia sala zanu daima. Tunatamani kuwa baraka kwa watu wa mahali tunakoishi na katika yote tunayofanya.

shukrani kwa wote kwa upendo wanu, msaada na kutukumbuka wakati wa jubilei yetu.

***Sr. Mini Pallipadan na Sr Mini Vadakkumchery, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Region ya Zagabria

# Miaka 125 ya uwepo wa ASC huko Bihać

### Bosnia na Herzegovina



Siku ya Jumamosi Juni 8, 2019 huko Bihać, walifika Waabuduo Damu ya Kristo arobaini wa Region ya Zagabria, pamoja na mkuu wa Region Sr. Ana Marija Antolović, walikuja kusherehekea maadhimisho ya miaka 125 ya uwepo na utume wa ASC katika mji huu. Kati ya wale waliokuwepo walikuwa masista kadhaa ambao katika miaka iliyopita waliishi na kufanya kazi huko Bihać.

Katika adhimisho hili pamoja na masista walikuwepo pia wageni wengi na wanaparokia ya Mt. Antoni wa Padua huko Bihać, pamoja na paroko na paroko msaidizi. Mans. Marko Semren, askofu msaidizi wa Jimbo la Banja Luka, aliongoza adhimisho la Misa pamoja na mapadri wengine waliotoka maeneo mbalimbali ya Region. Wakati wa Misa kwaya ya parokia iliimba pamoja na Pelikan, kwaya ya ASC chini ya uongozi wa Sr. Damiana Kovacević na kusindikizwa kwa kinanda kilichopigwa na Sr. Domagoja Ljubicić.

Baada ya Misa takatifu lilifuata tukio la kusherehekea katika ukumbi wa shule ya zamani ya ASC huko Bihać, iliyochukuliwa na serikali ya kikomunisti baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Sr. Ljubica Radovac aliongoza mipango ukumbini na kuwasalimu wageni.

Mwanzoni mwa mpango Sr. Blanka Šturm, mkuu wa jumuiya ASC ya Bihać, aliwakaribisha wale waliokuwepo kwa maneno haya: "Jubile ni zaidi ya kumbukumbu ya miaka 125 iliyopita. Sherehe hii kwetu sisi Masista ina maana kubwa sana, kifungo kinachotuunganisha na masista wengi waliotutangulia, ambao walijenga historia, walitengeneza njia na kujenga mtindo wa maisha ili kueneza maadili tunayopata, kuhifadhi na kutafuta kukuza tunu hizi ambazo bado tunazirithi, tudumu na kutafuta uwezekano wa kuziendeleza katika wakati wetu kulingana na uwezo wetu. Sherehe ya jubilei ni fursa ya kukutana na kufahamu zaidi kuhusu jumuiya yetu ASC, ili kutambua na kujali tofauti zetu na kuweza kutambuliwa kama wajenzi wa dunia bora. Mwingiliano wa tamaduni mbalimbali na mazungumzo ya kidini, yamekuwa ni tunu ambazo masista katika nchi hii wamezikuza tangu mwanzo wa kuwepo kwao, hali ya mapokezi wazi ni ishara ya nguvu na endelevu katika historia yetu. Asanteni kwa uwepo wenu na ushiriki, ambao unathibitisha heshima yetu. Nawakaribisha wote. Mpango huo utakuwa safari kupitia historia kati ya kumbukumbu za uwazi na ushirika. Nawashukuru wote kwa ushirikiano wenu wa thamani katika kuandaa jubilei hii, pamoja na kushiriki katika mpango huu."

Mpango wa tukio la sherehe hii lilikuwa na maudhui tofauti na shirikishi, katika sehemu ya muziki kwaya ASC Pelikan ilishiriki, kwaya mchanganyiko ya shule ya muziki wa Bihać na kwaya ya watoto wa Kituo cha Shule ya Katoliki huko Bihać. Michango ilitolewa na vijana wanafunzi wa shule ya muziki na sanaa: walitunga nyimbo



na kupiga kinanda na msichana mmoja aliyecheza kisanii alitufanya kuwa na muda wa pekee. Kwa njia ya uwasilishaji wa picha, pamoja na maandishi na muziki, ilitolewa historia fupi ya safari ya miaka 125 ya uwepo na kazi za ASC hapa Bihać.

Sherehe ya maadhimisho haya ilifadhiliwa na Serikali ya Shirikishoya BiH na Uongozi wa Manispaa wa Bihać. Ili kuheshimu miaka 125 ya kuwepo kwa ASC, jioni ya Juni 7, kwenye nyumba ya sanaa ya jiji, yalifunguliwa maonyesho ya picha, ambayo yanaweza kutembelewa kwa siku kumi. Maonyesho yalitayarishwa na wafanyakazi wa Nyumba ya sanaa kwa kushirikiana na profesa wa historia, Franjo Jurić, ambaye aliandika kitabu kidogo, Miaka 125 – Uwepo wa Waabuduo Damu ya Kristo Bihać, kilichochapishwa kwa ajili ya tukio hili.




***ASC wa Zagreb***

# Pamoja kwa ajili ya Maisha, Heshima na Haki za Kibinadamu

Kuanzia Machi 2017, kazi yangu ya utume ni ile ya kuwahudumia wanawake na watoto wao kwenye nyumba moja ya wanawake wakimbizi. Wanawake hawa hutoka hasa Asia ya Kusini-Mashariki: Vietnam, Cambodia, Laos, Tailandi, China, Philippine, Mongolia, Uzbekistan, n.k. Kwa ujumla ni vijana sana na ni wazuri na watoto wao pia ni wazuri sana, wakunjufu na wenye akili.wakiwa Korea huwa wana ndoto ya maisha bora, lakini kiuhalisia hayakuboreshwa kulinganishwa na yale waliyokuwa wanayaendesha katika nchi zao za kuzaliwa, kwa sababu walikuwa wahanga wa vurugu. Wamepoteza heshima yao ya utu na wanateseka kwa huzuni, ninawahurumia na kwa sababu hiyo nataka kuwahudumia.

Natumaini kuwa katika  kituo chetu watapata utulivu na amani, kwamba watapata nguvu za akili na kimwili na wataweza kujitunza wenyewe. Wakati mwingine ninawasindikiza hospitalini na kufanya mipango ya elimu kwa ajili yao: kujifunza Kikorea, maelekezo binafsi na ya kikundi, mafunzo ya sanaa, mafunzo ya yoga na kadhalika. Mipango inafaa na inawafanya kuwa na furaha, ikiwa wanapona kimwili na kiakili, watakuwa tayari kujitegemea wenyewe. Wanafanya kazi kwa bidii, lakini hawalipwa vizuri, kwa sababu hawazungumzi vizuri Kikorea, hata hivyo, wangefurahi kufanya kazi popote. Wangependa kuishi Korea na kuwa na ndoto ya maisha bora zaidi na mimi nataka kuwatetea na kuwasaidia hadi ndoto zao zitakapotimia kweli hapa Korea.

Maisha ya wanawake wahamiaji hapa Korea si ya uhakika, wanawake wengi wahamiaji walioolewa wanapaswa kuongeza muda wao wa kukaa kila mwaka au miezi sita na hii ina gharama kubwa, wana hati ya utambulisho wa kigeni lakini siyo kibali cha kutumia. Wanapaswa kutumia namba za kitambulisho cha nyaraka za watoto wao au waume zao, wakati wote ambapo hawana urai wa Korea, hata watoto wao hukumbana na ubaguzi wa kitamaduni shuleni na katika jamii na hali hii huongeza maumivu mara dufu kwa akinamama. Kwa bahati mbaya huku Korea wahamiaji ni wanyonge sana: wanawake, wageni na wale wasiozungumzi Kikorea. Utume wangu ni kuwa mikono na miguu ya Yesu kwao. Kwa kweli ninajaribu kuwapenda pamoja na watoto wao kama Yesu alivyonipenda mimi. Ninapoenda kukutana nao nahisi katika moyo wangu jinsi Mungu anavyowapenda, ni zawadi ya Mungu kwangu, kupitia kwao ninaonja haki, amani na muunganiko wa viumbe, kwa sababu wananipa uwezekano wa kujisikia kuwa ulimwengu ni familia kubwa. Wananisaidia kupanua namna yangu ya kufikiri, kujua tunu nyingi na maoni ya ulimwengu na labda wao pia wanaishi ukweli sawa na wangu ninaokumbana nao.

Ni kwa kufanya kazi nao na kuishi pamoja nao kama familia, kwamba ninaishi tunu za haki, amani na muunganiko wa viumbe unaostawishwa na JPIC yenyewe. Kituo chetu ni nafasi ya uwazi na ya ukaribishaji ambapo tunajaribu kutoa huduma nzuri kwa nguvu ya neno la Mungu.Wao ni watoto wapendwa wa Mungu na Yeye anataka kuwahudumia kupitia mikono na miguu yangu. Inanipa furaha na kuridhika kuona kuwa wana furaha na afya, hii inatosha kwangu kuishi maisha yangu ya wakfu kwa sababu ninaona kwamba Mungu ananipenda kama anavyowapenda wao. Hamu yangu ni kwamba waishi maisha yao kwa heshima na nadhani kwamba haya pia ni matarajio ya Mungu.

***Sr. Bo Hui Francesca Kang, ASC***



# Kalenda Shirika




**Julai 2** Sr. Nadia na Sr. Matija watarudi kutoka ziara ya kichungaji huko Australia.
**Julai 2-7** Sista Manuela atashiriki kikao cha tume ya mfuko wa fedha MDMHH atakuwa USA: hadi **14 Agosti**
**Agosti 25:** maadhimisho ya miaka 25 ya uwepo wa ASC huko Bellarussia - Sr. Bridget atashiriki kwenye sherehe

## Sikukuu za kuzaliwa: Tunashrehekea Maisha



### Julai

| | | |
|---|---|---|
| 50 miaka | | |
| **Sr. Ljiljana Marić** | 13/07/1969 | Zagabria |
| 60 miaka | | |
| **Sr. Patrizia Pasquini** | 10/07/1959 | Italia |
| 70 miaka | | |
| **Sr. Irena Zeba** | 14/07/1949 | Zagabria |
| 80 miaka | | |
| **Sr. Rosa (Bernardina) Panattoni** | 06/07/1939 | Italia |
| 90 miaka | | |
| **Sr. Maria Alteri** | 08/07/1929 | Italia |
| **Sr. Maria Antonia Capobianco** | 31/07/1929 | Italia |

### Agosti

| | | |
|---|---|---|
| 30 miaka | | |
| **Sr. Jyotji Nallamothu** | 14/08/1989 | India |
| 40 miaka | | |
| **Sr. Aldona Kala** | 25/08/1979 | Wrocław |
| 50 miaka | | |
| **Sr. Radegunda Kimaro** | 01/08/1969 | Tanzania |
| **Sr. Moly Pullan** | 13/08/1969 | India |
| 70 miaka | | |
| **Sr. Nicolina Rosa Pennucci** | 30/08/1949 | Italia |
| 90 miaka | | |
| **Sr. Maria Mossa** | 10/08/1929 | Italia |
| **Sr. Pauline Schneeberger** | 10/08/1929 | Schaan |
| **Sr. Helen Lindsey** | 13/08/1929 | USA |
| **Sr. Therese Marie Smith** | 18/08/1929 | USA |

## Nadhiri za kitawa



### 1 Julai 2019

**Miaka 50 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Brazili**
*Sr. Manoelina Marques Ferreira*

**Miaka 60 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Brazili**
*Sr. Maria José Dutra*
*Sr. Hellena Augusta Wallcott*
*Sr. Regina Nascimento*

**Miaka 65 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Brazili**
*Sr. Maria da paz Azevedo*
*Sr. Mônica Renilde Borsa Lima*
*Sr. Maria Serena do Vale*
*Sr. Clemens de Oliveira*

### 10 au 11 Agosti 2019

**Miaka 50 ya Nadhiri za Kitawa - Wichita Center**
*Sr. Vicki Bergkamp*

### 15 Agosti 2019

**Miaka 25 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Zagabria**
*Sr. Martina Katović*
*Sr. Melita Petra Kraševac*
*Sr. Nada Grgić*

**Miaka 50 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Zagabria**
*Sr. Branislava Garvan*
*Sr. Elvira Cvitković*
*Sr. Iluminata Antolović*
*Sr. Lucija Stipić*
*Sr. Mehtilda Čančar*
*Sr. Velimira Bosankić*
*Sr. Veronika Radoš*

## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 30/05/2019 | **Sr. Nina Rita Pagliaccio** | Italia |
| 08/06/2019 | **Sr. Giuseppina Ruo** | Italia |
| 14/06/2019 | **Sr. Lucia Gliaschera** | Italia |
| 16/06/2019 | **Sr. Teresina Vani** | Italia |


Gazeti la Kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*

***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 7, Julai/Agosti 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*